TANGAZO LA SERIKALI Na. 208 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA YA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (HIFADHI YA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI YA MWAKA 2023

Jina

TS Na 127 la tarehe 4/3/2022

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ya Mwaka 2023, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ya Mwaka 2022 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya Kifungu cha 3

2. Marekebisho yamefanyika katika kifungu cha 3 (1) (a) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta Kifungu hicho na kuweka mpangilio mpya wa aya ambapo iliyokuwa aya ya (b) kuwa aya ya (a) na zinazofuata kwa mtiririko huo.

Marekebisho ya Kifungu cha 4

3. Marekebisho yamefanyika katika kifungu cha 4 (1) (a) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta Kifungu hicho na kuweka mpangilio mpya wa aya ambapo iliyokuwa aya ya (b) kuwa aya ya (a) na zinazofuata kwa mtiririko huo.

Dodoma,
Machi, 2023

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB.),
*Waziri wa Nchi – OR- TAMISEMI*